


MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI - MEI 2021)



Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Machi-Mei (Masika) 2021

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua katika kipindi cha Machi - Mei, 2021, ushauri kwa wadau wa sekta na mamlaka mbalimbali kama vile Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Uvuvi, Utalii na Wanyamapori, Uchukuzi, Mamlaka za miji, Nishati, Maji na Madini, Afya pamoja na Menejimenti za Maafa. Baadhi ya mambo muhimu katika taarifa hii ni: -

- i. Mvua za Masika zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo).
- ii. Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.
- iii. Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza mapema katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2021 hususan katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini.
- iv. Vipindi vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza hususan katika mwezi Mei, 2021.

Athari zinazotarajiwa:

- i. Unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo unatarajiwa kuimarisha uzalishaji wa mazao mbalimbali ukiwemo mpunga.
- ii. Uwepo wa malisho na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo na wanyamapori unatarajiwa kupunguza migogoro baina ya wanyama na binadamu.
- iii. Matukio ya magonjwa ya mlipuko na wadudu waharibifu yanaweza kujitokeza kutokana na hali ya unyevunyevu na kutuama kwa maji.
- iv. Ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi na kuathiri shughuli mbalimbali hususan katika maeneo ya wachimbaji madini wadogo.
- v. Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kuambatana na mafuriko na kusababisha uharibifu wa miundombinu, shughuli za kijamii kuathirika, upotevu wa maisha na mali.

(I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA MACHI - MEI 2021

Msimu wa mvua za Masika ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa katika kipindi chote cha msimu (kama inavyoelezwa katika kipengele cha III cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hata hivyo, maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa Ziwa Viktoria yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Aidha, maeneo ya pwani ya kaskazini yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Msimu wa mvua za Masika unatarajiwa kuambatana na vipindi vya mvua kubwa hususan katika kipindi cha mwezi Machi.

1. *Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo)):*


Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2021 na kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Mei, 2021.

2. *Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):*

Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza mapema katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2021 na zinatarajiwa kuisha katika wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2021.

3. Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi na zinatarajiwa kuanza mapema katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2021 na kuisha katika wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2021.



Angalizo:

Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani.

(II) ATHARI NA USHAURI

Taarifa ya athari na ushauri imeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 15 na 16 Februari, 2021.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Katika kipindi cha Masika (Machi hadi Mei, 2021) hali ya unyevunyevu wa udongo na maji ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji inatarajiwa. Hata hivyo, hali hiyo ya unyevunyevu hususan katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki yanayotarajiwa

kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, inaweza kuathiri ukuaji wa baadhi ya mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mahindi, maharagwe na mazao ya mizizi.

Aidha, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo unaweza kujitokeza. Inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na vipindi vifupi vya mvua kubwa. Teknolojia ya uvunaji maji ya mvua izingatiwe ili kuhifadhi maji kwa matumizi ya baadae. Wakulima wanahimizwa kutafuta na kutumia ushauri wa wataalam wa kilimo ikiwa ni pamoja na maafisa ugani katika maeneo yao.

b) Mifugo na Uvuvi

Katika kipindi cha mvua za Masika 2021, hali ya malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa Ziwa Victoria ambayo yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Kwa upande mwingine, upungufu wa upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo unatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Magonjwa ya mifugo yanaweza kujitokeza katika msimu huu wa mvua za Masika. Hivyo, wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji, uvunaji maji ya mvua, kuhifadhi malisho kwa matumizi ya baadae pamoja na kupata ushauri wa kitaalam kutoka kwa maafisa ugani katika maeneo yao.

Upatikanaji wa maji ya kutosha katika maziwa, mito na mabwawa unatarajiwa kuchangia kuongezeka kwa chakula cha uzalishaji wa samaki. Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinavyotarajiwa kujitokeza vinaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu ya mabwawa ya samaki. Hivyo, wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa kitaalam kutoka kwa maafisa ugani katika maeneo yao na kutumia utabiri mahusus wa hali ya hewa wa kwenye maji.

c) Utalii na Wanyamapori

Hali ya malisho na maji kwa wanyamapori inatarajiwa kuongezeka hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Hata hivyo, kuharibika kwa

miundombinu pamoja na kuongezeka wadudu na magonjwa ya wanyamapori kunaweza kujitokeza hivyo, mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu ya barabara na maji na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wadudu na magonjwa ya wanyamapori.

d) Uchukuzi

Miundombinu ya usafirishaji inaweza kuathirika hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuchukua tahadhari ya hali ya hewa inayotarajiwa katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama vile reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege.

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, sekta ya usafirishaji hususan usafiri wa ardhini inaweza kunufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinavyoweza kujitokeza. Inashauriwa kuwa mipango ya uboreshaji wa miundombinu ifanyike kwa kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

e) Nishati, Maji na Madini

Viwango vya maji katika mabwawa vinatarajiwa kuendelea kuwa vya kuridhisha kutokana na mvua zilizonyesha katika msimu uliopita na kiwango cha mvua za masika kinachotarajiwa. Katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa madini, hatua za kuimarisha miundombinu zichukuliwe ili kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na mafuriko pamoja na maporomoko ya ardhi. Aidha, wadau wanasisitizwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji katika shughuli za kuchakata madini, uzalishaji wa umeme, matumizi viwandani na majumbani.

f) Mamlaka za Miji

Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hiyo inaweza kupelekea uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za miji zinashauriwa kuboresha mifumo ya kupitisha maji taka ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko. Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chache, mamlaka za miji pamoja na wananchi wanashauriwa kutumia muda huo kuboresha miundombinu na maeneo yanayozunguka makazi.

g) Afya

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, kuna uwezekano wa maji kutuama na kusababisha uchafuzi wa maji, kutokea magonjwa ya mlipuko. Aidha, mamlaka husika zinashauriwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa mapema na za kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuzingatia uwezekano wa uharibifu wa miundombinu unaoweza kujitokeza.

Upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu unaweza kujitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, hivyo hatua za kutibu maji kabla ya kutumia zizingatiwe. Hata hivyo, msisitizo unatolewa kwa mamlaka husika kutoa elimu ya afya kwa wananchi na kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kama vile kuzuia na kuharibu mazalia ya mbu.

h) Menejimenti za Maafa

Mafuriko, uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mali na maisha, mlipuko ya magonjwa pamoja na athari nyingine zitokanazo na mvua nyingi zinaweza kujitokeza. Hivyo, mamlaka husika na kamati za maafa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuzuia na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na vipindi vya mvua kubwa.

i) Vyombo vya habari

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mwenendo wa msimu pamoja na taarifa zilizo huishwa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii.

Vyombo vya habari vinashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa watoa taarifa wa sekta mbalimbali zinazotumia taarifa za hali ya hewa ili kuujulisha umma athari za kisekta. Aidha, vyombo vya habari vinashauriwa kuandaa na kusambaza makala za kitaaluma kwa kutumia lugha nyepesi kwa lengo la kuhabarisha jamii juu ya matumizi sahihi ya utabiri wa hali ya hewa.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyamapori, wasafirishaji, mamlaka za maji na afya kuendelea kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalam katika sekta husika.

(III) MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kati la bahari ya Hindi na joto la juu kidogo ya wastani linatarajiwa kaskazini mwa bahari ya Hindi kwa kipindi cha msimu wa mvua za mwezi Machi hadi Mei (Masika) 2021. Joto la bahari la wastani katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu unaovuma kutoka baharini kuelekea katika ukanda wa pwani. Aidha, joto la juu kidogo ya wastani kaskazini mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kusababisha upepo kuelekea katika eneo la pwani ya Somalia na hivyo kupunguza mvua katika baadhi ya maeneo ya pwani ya kaskazini.

Katika msimu wa mvua za Masika 2021, kunatarajiwa kuwepo kwa matlai (upepo wa mashariki) katika maeneo mengi. Hali hii inatarajiwa kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu Kaskazini Mashariki. Aidha, vipindi vichache vya migandamizo midogo ya hewa katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi vinatarajiwa kujitokeza hususan katika miezi ya Machi na Aprili, 2021. Hali hiyo inatarajiwa kuvuta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo na kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na maeneo machache ya nyanda za juu Kaskazini Mashariki. Aidha, katika eneo la kati la kitropiki la Bahari ya Pasifiki, joto la bahari linatarajiwa kuwa la chini ya wastani hivyo kuwa na mchango hafifu katika mvua za Masika, 2021 hapa nchini.

MWENENDO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2020 - APRILI, 2021) KWA MAENEO YANAYOPATA MSIMU MMOJA WA MVUA KWA MWAKA.

Mvua za *Msimu* zilizoanza mwezi Novemba, 2020 katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (mkoa ya Dodoma, Singida, Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa mkoa wa Morogoro) zinaendelea vizuri kama ilivyotabiriwa.

Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa

utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa.

Imetolewa: 18 Februari, 2021.

Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)